

Lengo la Maktaba ya Bunge la Marekani

Lengo la maktaba ni kuhakikisha kuwa
machapisho yanapatikana kwa urahisi na ni
ya manufaa kwa bunge na watu wa
Marekani na pia kuendeleza na
kuhifadhi makusanyo ya fani zote yaliyo
na maarifa na ubunifu wa kufaa vizazi vijavyo.

James H. Billington, Mkutubi wa Bunge la Marekani

Nchi Zinazohusishwa

- Angola
- Banada
- Botswana
- Buki
- Burundi
- Eritria
- Gaboni
- Gana
- Jibuti
- Kameruni
- Kenya
- Komoro
- Kongo (Jamhuri
ya Kidemokrasia)
- Lesotho
- Malaw
- Mayotte
- Morisha
- Msumbiji
- Namibia
- Tanzania
- Reunion
- Rwanda
- Senegali
- Swaziland
- Uganda
- Ushelisheli
- Zambia
- Zimbabwe



Jinsi ya kuwasiliana na ofisi

ya Nairobi Marekani:

Library of Congress Office, Nairobi

Unit 64110/LOC

APO, AE 09831-4110 USA

Katika Afrika:

U.S. Library of Congress Office

P.O. Box 1492, Village Market

00621 Nairobi Kenya

Nambari ya simu:

(254) 020-363-6148

Kipepesi: (254) 020-363-6321

Barua pepe: NAIROBI@LOC.GOV

www.loc.gov
www.lcweb.loc.gov/acq/ovop/nairobi

Machi 2006



**U.S.
LIBRARY
OF CONGRESS
OFFICE**

OFISI YA MAK TABA YA BUNGE LA MAREKANI
NAIROBI • KENYA

Mpango wa Ushirika wa Mapato

Katika mwaka wa 1992, Maktaba ya Bunge la Marekani ilianzisha Mpango wa Ushirika wa Mapato katika ofisi ya Nairobi, wa kupata vitabu vya Kiafrika pamoja na majarida, kwa maktaba shiriki ya kitaaluma. Huduma hii ambayo hupatikana Kenya, hutoa vitabu na majarida kutoka kwa nchi 29, yakiwamo majarida ya kitaalamu, magazeti katika nyanja za sayansi ya siasa, sayansi ya jamii, lugha, fasihi, sayansi ya uendeshaji wa viwanda, elimu, sayansi, historia, utamaduni, na sheria.

Vitabu na majarida yanayotolewa katika mpango huu huchaguliwa kwa uangalifu. Mionganini mwa vigezo vinyavyotumiwa wakati wa uchaguzi ni kama vile utafiti wa thamani, upatikanaji, utumainifu, na wakati mwafaka. Kwa orodha kamili ya maelezo kuhusu upatikanaji, rejea kwenye tovuti: www.loc.gov/acq/ovop/nairobi.

Katika mwaka wa 1997, ofisi ilianza kutoa huduma ya uchaguzi wa takwimu, haki za binadamu na makala ya kisheria kutoka kwa nchi 24 kwa bei iliyowekwa. Tazama tovuti iliyoko hapo juu kwa maelezo zaidi.



Taarifa ya Jumla

Ofisi ya Maktaba ya Bunge la Marekani ya Nairobi Kenya, ni moja kati ya ofisi sita za ng'ambo zinazosimamiwa na Kitengo cha Shughuli za Mapato ya Ng'ambo ya Kiafrika/Kiasia cha maktaba. Ofisi hizi hupata, huorodhesha, huhifadhi na kugawa nyenzo hizi za maktaba na utafiti kutoka nchi ambazo kupatikana kwao ni haba hasa kuititia mbinu za upataji za kawaida.

Ofisi ya Nairobi husanya nyenzo kutoka nchi 29 za Afrika ya kupakana na Jangwa la Sahara, Afrika ya kat, magharibi, mashariki na kusini. Lengo la ofisi hii ni kuimarisha makusanyo ya utafiti yaliyoko kwenye maktaba ya Bunge la Marekani kwa kutegemea wingi wa kibibliografia ulio na manufaa unaotoka kwa nchi hizi.

Ofisi ya Nairobi ilifungua milango yake mwaka wa 1966 ikiwa kama Ofisi ya Mpango wa Kitaifa wa Mapato na Orodha ili kuihudumia maktaba ya Bunge la Marekani ikijihuisha na machapisho ya Kiafrika. Kwa miaka mingi, nchi nyingi zilliongezwa na kusababisha kuanzishwa kwa Mpango wa Ushirika wa Mapato wa vitabu na majarida mwaka wa 1992.

Machapisho yanayopatikana ya maktaba ni pamoja na vitabu, majarida, kabrasha, vikasha vya diskii, ramani, mabango, mipangilio ya sauti ya ala za muziki, na mengineyo. Machapisho mengi hununuliwa na ofisi lakini karibu nusu ya machapisho haya inapewa kama zawadi kutoka kwa takriban sehemu 2000.



Mwelezo wa Maandishi ya Tarigia za Kiafrika Unaotolewa Kila Baada ya Miezi Mitatu.

Tangu mwaka wa 1991, Ofisi ya Nairobi imetoa mwelezo wa maandishi ya tarigia ya majarida ya Kiafrika, yanayochapishwa na vyuo vikuu mbalimbali vya Afrika, mashirika mbalimbali, na hata mawakala mbalimbali ya kiserikali.

Makusanyo haya teule, huwezesha maandishi haya, ambayo ni ya kimsingi na ambayo yamechapishwa kibiashara au yasiyochapishwa kibiashara, na ambayo wakati mwingine ni nadra kupatikana, kufikika. Maandishi haya yenye mvutio wa kisomi, ni muhimu kwa masomo ya maswala mengi ya Kiafrika.

Kijilografia, maeneo yote ya Afrika yamewakilishwa kwenye mwelezo huu. Mwelezo ulichapishwa kwa nakala kuanzia 1991-2002, lakini sasa unapatikana tu kwenye mtandao wa kompyuta: <http://memory.loc.gov/misc/qsihtml>.